USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE

TZ21 21ST CENTURY BASIC EDUCATION PROGRAM

# MWONGOZO WA KUSOMA KWA UFAHAMU



**Februari 2015**

**PROGRAMU YA ELIMU YA MSINGI YA TZ 21**

# Shukrani

Mafunzo haya ya ziada ya Kusoma kwa Ufahamu na mwongozo huu kwa walimu wa darasa 1 na 2 ni matokeo ya msaada wa watu wa Amerika kupitia ufadhili wa Shirika la Misaada ya Kimataifa ya Mendeleo la Marekani (USAID) kwa Programu ya Elimu ya Msingi ya TZ21. Msaada huu wa watu wa Marekani unalenga kujenga uwezo wa watoto wa Tanzania kielimu. Msaada huu unakusudia kuboresha stadi za usomaji za wanafunzi katika hatua za awali wanapoanza kusoma shuleni ili kuinua matokeo mazuri ya usomaji yanayotarajiwa kwa watoto wote wa shule za Mtwara na Zanzibar. Programu ya Elimu ya Msingi ya TZ21 inatambua mchango wa kipekee uliotolewa na Amy Pallangyo-Mtaalam Mshauri wa TZ21 katika kutayarisha mwongozo huu wa mafunzo. Pia shukrani ziwaendee wafanyakazi wataalamu wa TZ21 na MOEVT kwa kuendesha mafunzo kwa wawezeshaji wa mafunzo ngazi ya wilaya kwa mkoa wa Mtwara na Zanzibar.

Hivyo basi shukrani za pekee zinatolewa kwa Shirika la Misaada ya Kimataifa ya Mendeleo la Amerika (USAID) kwa kufadhili kazi hii.

Maoni yaliyomo katika mwongozo huu ni ya waandishi. Hayawakilishi kwa namna yoyote ile maoni au msimamo wa Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) au Serikali ya Marekani (USA).

Kimetolewa na kuchapishwa kwa ufadhili wa UASID wa Programu ya Elimu ya Msingi (TZ21) kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Tanzania Bara na Zanzibar

# Malengo

Malengo ya mwongozo huu  wa Kusoma kwa Ufahamu ni kuwapatia walimu msaada maalumu, mifano, na mikakati ya kuboresha uwezo wa usomaji kwa ujumla na ufahamu kwa wanafunzi. Mwongozo huu utatoa:

1. Historia fupi na maelezo ya usomaji, kufundisha kusoma na kusudi maalum la kufundisha ufahamu,
2. Misingi ya ufundishaji fanisi wa kusoma kwa ufahamu kwa wanafunzi wa madarasa ya chini kwa kutumia mazingira na zana za kawaida,
3. Jinsi ya kufundisha kusoma katika kundi kubwa,
4. Jinsi ya kufundisha kusoma katika vikundi vidogo, na
5. Jinsi ya kuwasaidia wanafunzi wanaosoma kwa shida.

Walimu wanaweza kutumia taarifa zilizomo katika mwongozo huu kuboresha maarifa yao ya jumla ya kufundisha kusoma, kujifunza mambo yanayopaswa kuangaliwa katika ufundishaji bora wa kusoma na kuelewa jinsi ya kutumia matini waliyo nayo katika madarasa yao ili kubuni na kufundisha kwa ufanisi kusoma kwa ufahamu. Aidha, walimu wanaweza kutumia sehemu ya mwongozo huu inayohusiana na kuwasaidia wasomaji wanaosoma kwa shida  pamoja na kutumia dodoso za TZ21 za kufanya tathmini endelevu ili kukidhi mahitaji ya msomaji anayesoma kwa shida.

## Yaliyomo                                                    ukurasa


**Shukrani** ........................................................................ i

**Malengo** ........................................................................ ii

**Maelezo Kuhusu Usomaji** ........................................................ 1

Majumuisho: Kufanikisha Kusoma kwa Ufahamu ........................................2

**Mbinu Endelevu za Usomaji** ........................................................ 3

Kusoma – Chekechea/Awali: ........................................................3

Kusoma– Darasa la Kwanza: ........................................................4

Kusoma– Darasa la 2: ........................................................5

**Misingi ya Kufundisha Kusoma kwa Ufahamu** ........................................ 6

Stadi za Kusoma……………………………………...……...……………….……………6

Kuonesha Mfano wa Usomaji Fanisi**………………………………………………...….7**

Masomo ya Kusoma Kwa Ufahamu ........................................................7

Masomo Mengi kwa Matini Moja ........................................................8

**Kabla, Wakati na Baada: Mchakato wa Somo la Ufahamu** ........................ 9

Mambo ya Kufanya na Kutofanya Wakati wa Kusoma ....................................10

Mambo ya Kufanya na Kutofanya Wakati wa Usomaji ....................................11

Baada ya Kusoma: Vitu vya Kufanya na Vitu vya Kutofanya ............................12

**Kupanga kwa ajili ya Ufundishaji wenye Ufanisi wa Kusoma kwa Ufahamu.. 13**

**Kutoa msaada kwa wanafunzi wenye shida ya kusoma.** ................................ **14**

**VIAMBATISHO: Mifano ya Masomo ya Kusoma kwa Ufahamu** .................... **15**

Mfano wa Andalio la Somo # 1: Onesho la Mfano kwa Wasomaji Wanaoanza ............15

Mfano wa Andalio la Somo # 2: Kufundisha Kikundi Kizima cha Wasomaji Wanaoanza ........................................................16

Mfano wa Andalio la Somo # 3: Onesho la Mfano kwa Wasomaji Wanaoibukuia .......17

Mfano wa Andalio la Somo #4: Usomaji katika Kikundi kidogo. Msomaji anayeibukia 18

Mfano wa Andalio la Somo #5: Kuonesha Mfano kwa Wasomaji Mahiri ....................19

Mfano wa Andalio la Somo #6:  Kufundisha Kundi Zima la Wsaomaji Mahiri ...............20

## Maelezo Kuhusu Usomaji

Uwezo wa kusoma ni uwezo wa kuelewa na kuwasilisha maudhui yaliyo kwenye matini. Kusoma kunahusisha hatua nyingi na ngumu. Utaratibu huu una hatua zinazotegemeana katika kumwandaa mwanafunzi kusoma kwa ufahamu.

**Sehemu ya 1: Utambuzi wa Sauti -** Kuwa msomaji huanza na msingi wa kuelewa sauti zinazounda maneno na herufi. Hatua hii hufanyika shuleni na wanafunzi wadogo sana (Elimu ya awali – darasa la kwanza), kwa kuchunguza maneno ambayo wanafunzi wanayasikia na kuyazungumza kwa uelewa (Utambuzi wa Sauti), kisha kurasimisha sauti hizo kwa kutumia kadi za herufi na kufanya mazoezi ya kutambua sauti na herufi wanazozijua (utambuzi wa sauti na herufi).

**Sehemu ya 2: Kuhusisha sauti na herufi:** Utambuzi wa sauti hutambulishwa kwa wanafunzi kabla ya uwezo wa kubaini herufi, lakini walimu hawapaswi kusubiri wanafunzi wajifunze utambuzi wa sauti kwanza ndipo waanze kufundisha uhusiano wa sauti na herufi. Vipengele hivi viwili vinapaswa kufundishwa kwa wakati mmoja.

**Sehemu ya 3: Msamiati**

**Msamiati uliozoeleka-** Wanafunzi hutumia uelewa wao wa herufi na sauti kuanza kubaini maneno waliyozoea ambayo wanaweza kuyatambua, kuyakariri, na kuyasoma. Haya ni maneno rahisi ambayo wanafunzi hukutana nayo mara kwa mara katika maisha yao ya kila siku. Mara nyingi ni maneno yenye silabi moja au mbili na ni maneno ya msingi ya lugha ya mazungumzo na ya kuandikwa (na, ya, kwa, sasa, yule, nani, mama, baba, dada, kaka, kuku nk).

**Msamiati wa Kusimbua-** Baadhi ya maneno ni magumu na hayafahamiki kwa wanafunzi wachanga. Katika mazingira ya namna hii, wanafunzi hutumia uwezo wao wa utambuzi wa alama ya sauti (foniki) kutamka (kusimbua) maneno hayo, huhusisha herufi/kundi la herufi na sauti kutambua neno, na kisha kuelewa maana ya neno hilo.

**Kumbuka: Msamiati - Umuhimu wa Kuelewa:** Ikiwa wanafunzi wanakutana na maneno waliyoyazoea au maneno ya kusimbua, ni muhimu kwao kuchunguza maana ya maneno hayo, ili kuweza kuwa na wajuzi wa msamiati . Ingawa wanafunzi wanaweza kutamka maneno, kama hawataweza kujadili maana ya maneno hayo, watakuwa hawajaanza kusoma. Utambuzi wa sauti ya/kutamka neno, bila kujua maana ya neno hilo, haisadii kukuza uwezo wa mwanafunzi kusoma.

**Sehemu ya 4: Ufundishaji wa Kusoma kwa Ufahamu** – Kufundisha Kusoma kwa Ufahamu hutokea pale ambapo wanafunzi huanza kutumia uelewa wao wa utambuzi wa alama za sauti (foniki) na msamiati, kusoma hadithi na habari, na kuelewa wanachokisoma. Kupambanua maana yake ni kuelewa. Kwa hiyo lengo la kufundishia Kusoma kwa ufahamu, ni kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapata ufahamu kamili wa kile wanachokisoma. Hata kama mwanafunzi anaweza kutamka neno, kutaja msamiati anaoujua, na hata kusoma vizuri kwa sauti - hii haimaanishi kuwa wanaelewa wanachokisoma. Ufahamu wa kusoma hutokea tu kupitia mchakato wa kupeana na kujadili kile walichosoma, na uthibitisho wa kuwa wamefahamu hutokea tu wakati mwalimu anapoongea na wanafunzi kuhusu walichosoma na kubaini kama wanaelewa matini.

**Sehemu ya 5: Ufasaha ni Matokeo ya Mwisho: -** Inapotokea wanafunzi wanaweza kutambua maneno wanayoyajua, kutamka maneno wasiyoyajua, kuelewa maana ya maneno hayo (msamiati), na kuelewa matini wanayosoma (ufahamu) - basi hapo tunaweza kusema kuwa wanafunzi hao wanasoma kwa fasaha. Ufasaha si stadi ya kufundishwa. Ufasaha ni matokeo ya kufundisha stadi. Ufasaha unajumuisha: 1) wanafunzi kuwa na uwezo wa kusoma kwa kasi sahihi (siyo kasi sana au polepole sana), na 2) wanafunzi kuwa na uwezo wa kusoma kwa sauti sahihi (kuonyesha kuwa wanaelewa wanachokisoma). Ili kusoma kwa kasi sahihi na sauti sahihi, wanafunzi ni lazima wawe na uwezo wa kuelewa wanachokisoma. Mazoezi ya ufasaha ni muhimu katika kusaidia maeneo mengine yote ya kufundishia kusoma, lakini yenyewe peke yake, hayana uwezo wa kumjenga msomaji ambaye anaweza kusoma matini na kuyaelewa. Ufasaha ni mchakato tu wa kufanya mazoezi ya stadi zilizopatikana kwenye utambuzi wa sauti na herufi, msamiati, na kwenye ufundishaji kusoma kwa ufahamu. Kama wanafunzi hawawezi kuelewa wanachokisoma, mazazoezi ya ufasaha huwasaidi kidogo sana kuwa wasomaji mahiri.

## Majumuisho: Kufanikisha Kusoma kwa Ufahamu

1. Ufahamu maana yake ni kuelewa maana kamili ya matini iliyosomwa.
2. Ufahamu hufanikishwa kwa njia ya kusoma, na kufanya majadiliano ya kilichosomwa.
3. Kusoma kwa sauti hakusaidii kujenga ufahamu wa matini.
4. Ufahamu wa matini hupatikana endapo wanafunzi watasoma kimya, na kisha kujadili walichokisoma ili kupata maana ya matini.
5. Walimu wanashauriwa kutumia mbinu maalum ili kusaidia kuinua na kuboresha Kusoma kwa Ufahamu .

6. Ufundishaji wa utambuzi wa alama za sauti (foniki) na Msamiati hausaidii kujenga uelewa wa matini. Ni lazima mambo hayo mawili yaambatane na mafunzo maalum ya ufahamu.
7. Ufasaha si miongoni mwa mbinu za ufundishaji wa kusoma, bali ni mazoezi ya stadi za kusoma ambayo yanasaidia ufundishaji wa kusoma. Si vema Ufasaha kutazamwa kama njia ya kufanya kuwa msomaji. Badala yake, inapaswa kutazamwa kama fursa ya kufanyia mazoezi stadi zilizojengwa kwenye utambuzi wa sauti, utambuzi wa alama za sauti, msamiati, na ufundishaji wa kusoma ufahamu.

## Mbinu Endelevu za Usomaji


Katika ufundishaji wa kusoma duniani, wataalam huzungumzia hatua mbili za usomaji darasani: 1) Kujifunza Kusoma, na 2) Kusoma ili Kujifunza. Katika hatua ya 1 ya kujifunza kusoma wanafunzi hushirikishwa katika kujifunza utambuzi wa sauti kuhusisha sauti na herufi, maneno na msamiati uliozoeleka na kufundisha Kusoma kwa Ufahamu kwa walengwa.

Hatua hii ya awali ya *Kujifunza Kusoma* inaanzia katika darasa la awali/chekechea hadi darasa la pili. Katika hatua ya pili, ya *Kusoma ili Kujifunza*, wanafunzi wanashirikishwa kutumia na kujizoeza kutumia stadi zao za kusoma kadri wanavyojifunza maudhui ya somo darasani (Kiswahili, Mathematics, Sayansi, na Sayansi Jamii). Hatua hii ya ufundishaji wa kusoma ili kujifunza huanzia Darasa la tatu na kuendelea hadi sekondari.

**Katika hatua ya 1- Kujifunza Kusoma,** wanafunzi huendelea kujenga stadi za kusoma kwa kupitia hatua mbalimbali za kuwafanya wawe na utayari wa kuanza kusoma.

### Kusoma – Chekechea/Awali:


Katika darasa la Chekechea/Awali, wanafunzi wanahitaji zaidi uzoefu mpana katika kuzungumza sauti na maneno ambayo wamezoea kuyasikia (Utambuzi wa sauti). Pia wanafunzi wanahitaji uzoefu mpana katika kutambua alama za sauti au herufi (foniki). Hapa ndipo pia wanafunzi wanajifunza kutambua maneno ambayo ni kawaida waliyozoea kusikia na kuyaona kila siku (Msamiati). Mwisho, kwa vile wanafunzi bado hawajawa tayari kusoma wenyewe, mwalimu atawaongoza kwa kuwaonesha mwenendo bora wenye ufanisi wa usomaji kwa kuwasomea kwa sauti wanafunzi wa umri unaohusika kwa kutumia picha, vitabu na kuwashirikisha wanafunzi kuongea kuhusu matini aliyosoma mwalimu (Kuonesha na kupata mrejesho wa usomaji toka kwa wanafunzi). Sio jambo sahihi katika hatua hii mwalimu kutarajia wanafunzi kusoma wenyewe. Mwalimu atawapa wanafunzi changamoto kwa kuanzisha majadiliano ya matini aliyowasomea kwa sauti, na kutumia jitihadi nyingi kusaidia wanafunzi kuelewa kuwa ***kusoma maana yake ni kuelewa ulichosoma.*** Chati hii hapa chini inaonesha jinsi mwalimu atakavyotumia muda katika kufundisha kusoma kwa darasa la Chekechea/Awali




## Kusoma– Darasa la Kwanza:


Katika darasa la kwanza, wanafunzi wanaweza kuanza kusoma matini rahisi wao wenyewe. Mwalimu bado anahitaji kutumia muda wa kutosha kuwafundisha utambuzi wa sauti na kutambua alama za sauti au herufi na pia kuendelea kuwafundisha msamiati (katika hatua hii sio tu kuwafundisha maneno waliyoyazoea lakini pia hata kusoma maneno wasioyazoea) . Ni katika eneo la usomaji wa matini ambapo ufundishaji kwa darasa la kwanza hubadilika. Mwalimu ataendele kuonesha mwenendo bora wa usomaji kwa wanafunzi, lakini pia wanafunzi wataanza kusoma matini rahisi kwa kujitegemea, katika vikundi vidogo vidogo, na katika kundi kubwa. Kwa kuongezea, wanafunzi wanakuwa katika nafasi nzuri ya kutoa mrejesho wa kile alichowasomea mwalimu wao na kile walichosoma wenyewe. Na kwa sababu hiyo muda wa wanafunzi kuweza kutoa mrejesho wa usomaji unaongezeka.

**Kutoa majibu kutokana na matini-**kwa kupitia majadiliano, maswali, na hata uchoraji wa picha rahisi- ndipo wanafunzi hujifunza vizuri zaidi kuelewa walichosoma. Wakati huohuo baadhi ya walimu hutia shaka kuwa wanapoteza muda wa kufundisha, ni hakika hii ni sehemu muhimu katika ufundishaji wa kusoma, na ni lazima kutoa muda wa kutosha katika aina hii ya kazi kwa kila wakati wanafunzi wanaposoma. Katika darasa la kwanza, Lengo muhimu la kufundisha kusoma ni kumsaidia mwanafunzi kuelewa kuwa kuna ***mfumo wa mchakato wa kusoma na kuelewa.*** Chati hapa chini inaonesha jinsi mwalimu atakavyotumia muda katika kufundisha darasa la kwanza.




## Kusoma– Darasa la Pili:

Katika Darasa la pili, ufundishaji kusoma hubadilika kwa njia kadhaa. Hapa wanafunzi hawahitaji kufundishwa utambuzi wa sauti. Kwa nyongeza, ufundishaji wa kutambua alama za sauti au herufi pia kwa kiwango kikubwa unakuwa umekamilika- na utatizamwa kama marudio na mazoezi ya stadi, na sio mafundisho mapya. Hii ni kwa sababu vipengele vya kufundisha usomaji kimsingi vimekamilika, wanafunzi sasa wanaweza kutumia muda wao mwingi katika kujifunza kusoma maana ya maneno mapya na magumu zaidi, kusoma matini ngumu zaidi kusoma wenyewe na kujibu matini kwa namna ngumu zaidi. Katika hatua hii wanafunzi wanaweka katika **vitendo stadi walizonazo tayari .***Ni katika darasa la pili, ambapo kufuata usomaji wa ufahamu kiufasaha kwa kujitemea kuna kuwa bora zaidi*. Wanafunzi wanaweza kusoma na kuelewa matini ngumu (Sentensi nyingi zenye maudhui au maana inayofanana),wanatumia uzoefu katika ufasaha wao kuwasaidia kutumia vipengele vitano ili kuwa wasomaji mahiri. Chati duara hapa chini inaonesha jinsi mwalimu atakavyotumia muda wa ufundishaji kusoma kwa darasa la pili.




## Misingi ya Kufundisha Kusoma kwa Ufahamu

### Stadi za Kusoma

Wasomaji mahiri huleta tabia na stadi za namna fulani wamapokuwa wanasoma. Kuna stadi maalumu ambazo msomaji mahiri huwa nazo, na stadi hizi lazima zijengwe kwa wanafunzi kupitia ufundishaji maalumu wa ufahamu wa kusoma. Baadhi ya stadi za msomaji mahiri ni pamoja na uwezo wa:

1. Kutabiri nini kinaweza kutokea katika matini, na kuangalia usahihi wa utabiri wao wakati na baada ya kusoma
2. Kaibaini wahusika na kufahamu uhusika wao
3. Kutambua tatizo na suluhisho katika hadithi
4. Kubaini chanzo na matokeo ya wahusika na matukio
5. Kuelewa mtiririko wa hadithi
6. Kusimbua maneno yasiyofahamika yaliyomo kwenye hadithi
7. Kutumia picha, chati au grafu kuelewa matini vizuri
8. Kusoma na kuelewa taarifa iyoko katika matini
9. Kuelewa tofauti kati ya maoni na ukweli katika matini
10. Kurudia kusoma ili kuelewa dhana ngumu au mawazo magumu
11. Kuuliza maswali yanayohusiana na matini wakati na baada ya kusoma
12. Kujibu maswali yanayohusu matini iliyosomwa
13. Kufupisha mawazo makuu yaliyo kwenye matini yoyote

Hizi ni stadi za msingi za msomaji mahiri, na wasomaji fasaha hutumia stadi hizi kiasili wanapokuwa wanasoma. Hata hivyo, stadi hizi si za asili kwa wasomamaji wanaoanza na wasomaji wachanga, ni lazima zijengwe kupitia ufundishaji wa ufahamu wa kusoma. Katika somo lolote la ufahamu, walimu huchunguza matini mapema ili kubaini stadi za msingi za kusoma (zilizotajwa hapo juu) ambazo zinaweza kushughulikiwa na kupewa msukumo kupitia mchakato wa kusoma. Si kila matini inafaa kukuza kila stadi. Ni pale tu mwalimu

anapoweza kuhusianisha matini na stadi ndipo wanafunzi watakuwa na uwezo wa kujenga stadi hizi muhimu baada ya muda.

Ili kujenga stadi hizi za msingi katika ufahamu wa kusoma, kuna aina mbili za masomo ya msingi ambazo ni lazima zizingatiwe katika kufundisha ufahamu wa kusoma: Kuonesha mfano wa usomaji fanisi, na kuwashirikisha wanafunzi katika masomo ya Kusoma kwa Ufahamu.

### Kuonesha Mfano wa Usomaji Fanisi

Huu ni mchakato ambapo walimu husoma kwa sauti ili kuonyesha jinsi msomaji mahiri anavyosoma, na kuonyesha stadi maalumu na muhimu za kusoma ikiwa ni pamoja na stadi ziliotajwa hapo juu. Walimu wanaofundisha madarasa ya shule za msingi kwa kawaida hutumia matini rahisi na zenye mvuto wa hali ya juu; vitabu vya hadithi, simulizi za kale, na hadithi zinazohusu watoto wadogo – ili wanafunzi waweze kuhusianisha na maisha yao binafsi. Wakati wa kutoa mfano wa kusoma kwa ufanisi, walimu hufikiri kwa sauti kuhusu nini kinaendelea katika ubongo wao wakati wanapokuwa wanasoma - hujihoji wenyewe kuhusu nini wanasoma, hurudia kusoma maeneo waliyoona ni magumu, huangalia picha ili kuelewa zaidi kuhusu matini, na kuhusianisha na maarifa yao ya awali wanapokuwa wanasoma. Katika kuonyesha namna ya kusoma kwa ufanisi, mwalimu huwasaidia wanafunzi kuelewa kusoma na huhitaji kufikiri mchakato hai, na sio fumbo.

Walimu lazima wajiandaae kwa ajili ya somo la mfano kwa:

1. Kusoma matini kwa sauti mara nyingi kwa lengo la mazoezi ya kujenga ufasaha na sauti ya msomaji mahiri
2. Kupanga ni namna gani mwalimu atafikiri kwa sauti katika kila ukurasa wa matini kwa ajili ya wanafunzi. Walimu wanapaswa kuandika maelezo kuhusu namna watakavyosoma na kufikiri kwa sauti katika kila ukurasa.

Zifuatazo ni baadhi ya tabia za usomaji ambazo walimu wanapaswa kuonesha wakati wa kusoma. Mfano wa namna ya kusoma kwa ufanisi ni:

1. Kutabiri nini kitatokea katika matini
2. Kujiuliza maswali mwenyewe ili kupata ufahamu
3. Kutumia picha kupata ufahamu
4. Kurejea kurasa na kurudia kusoma ili kupata ufahamu

## Masomo ya Kusoma Kwa Ufahamu

Masomo haya hufanyika wakati wanafunzi wanapokuwa wanasoma na kujibu matini ili kupima na kujenga ufahamu wa walichosoma. Wanafunzi wanapaswa kusoma matini **zinazolingana na umri na ngazi zao za kusoma**. Wakati wa masomo ya kusoma kwa ufahamu, wanafunzi **husoma kimya** hali ambayo huongeza uwezo wao wa kuelewa wanachosoma. Pia, hujibu walichosoma kwa njia ya maswali, majadiliano, na kutengeneza vitu rahisi (hususani michoro au kusimulia upya hadithi) kuonyesha kwamba wameelewa

walichosoma. Masomo ya Kusoma kwa ufahamu yanaweza kufanyika kwa namna mbilli – Ufundishaji katika vikundi vidogo na ufundishaji wa kundi zima.

Ufundishaji wa ufahamu wa kusoma katika vikundi hufanyia katika makundi ya wanafunzi 6 -8 na huwapaswa kusoma matini inayofanana, wakisaidiwa na mwalimu. Kusoma katika makundi madogo ni muhimu kwa wanafunzi kwa sababu wanaweza kuuliza maswali na kupata msaada wa mwalimu wanapoona ugumu katika matini.

Ufundishaji wa ufahamu wa kusoma katika kundi zima unafanyika kwa darasa zima ambapo wanafunzi wote husoma matini ya aina moja (inayofanana), na mwalimu hufanya kazi ya kufuatilia. Kusoma katika kundi zima ni mbinu ya ufundishaji inayoweza kutawalika na pia hutoa fursa nzuri kwa wanafunzi kusoma pale ambapo kuna matini chache darasani.

Iwe wanafunzi wanasoma katika vikundi au kundi zima, mchakato wa kuandaa na kutekeleza masomo haubadiliki. Hujumuisha kuandaa wanafunzi kabla ya kusoma, kusaidia wanafunzi wakati wa kusoma, na kujibu matini baada ya kusoma.

## Masomo Mengi kwa Matini Moja

Waalimu wanaweza kutumia matini moja mara nyingi wakati wa kufundisha. Kwa mfano, walimu wanaweza kutumia matini moja kwa siku tatu mfululizo, katika utaratibu ufuatayo:

**Siku ya 1 –** Somo la Mfano: Kwanza, mwalimu husoma matini kwa sauti, akitoa mfano wa tabia za usomaji fanisi.

**Siku ya 2 –** Usomaji katika kundi zima: Walimu wanaweza kutumia matini iliyosomwa siku ya kwanza kuisoma tena siku inayofuata kwa ajili ya wanafunzi kusoma katika kundi zima. Kwa kufuata mfano wa kusoma na kundi zima, walimu huwasaidia wanafunzi katika hatua za mwanzo ili wanafunzi wajiamini kwamba wanaweza kusoma wenyewe, na kujifunza kufahamu wanachosoma.

**Siku ya 3 –** Ufundishaji kusoma katika vikundi. Baada ya kusoma matini kwa sauti (Somo la mfano), na kisha kusoma katika kundi zima (usomaji wenye usaidizi wa hali ya juu), sasa wanafunzi wanaweza kusoma matini hiyo hiyo katika vikundi, ambapo hufanya kazi kwa kujitegemea zaidi wakati na baada ya kusoma.

Kusoma matini hiyo hiyo katika somo la mfano, na katika makundi mbalimbali, walimu huwapa fursa wanafunzi kuona matini hiyo mara nyingi na fursa ya kurudia kusoma matini ambayo wanaijua. Unapowataka wanafunzi wachanga wasome matini wanayoifahamu, walimu huwa na uhakika kwamba wanafunzi wanajiamini, na wanausaidizi wa kutosha kuwafanya wafahamu wanachosoma. Kadiri wanafunzi wanapokuwa wanaimarika katika stadi za kusoma, kurudia kusoma matini ile ile kunaweza kupunguzwa kadiri muda unavyosonga mbele, na wanafunzi wanaweza kusoma kwa kujitegemea zaidi na kwa mafanikio zaidi.

## Kabla, Wakati na Baada: Mchakato wa Somo la Ufahamu

### Kabla ya Kusoma

Kabla wanafunzi hawajaambiwa wasome, ni muhimu mwalimu kuwaandaa. Hii inaweza kukamilishwa kwa kupitia hatua chache zifuatazo:

1. Tambulisha jina la matini watakayosoma
2. Uliza maswali machache ili kuchochea wanafunzi kutabiri yaliyomo katika matini watakayosoma
3. Husisha matini mpya na matini nyingine ambazo wanafunzi walikwishasoma hapo kabla
4. Waambie wanafunzi matarajio yako kwao kuhusiana na matini

Mfano anaoweza kuutumia mwalimu katambulisha matini ni kama ifuatavyo:

> *Leo tutasoma hadithi inayoitwa Sungura na Kobe. Unaweza kuona jina la kitabu pamoja na picha yake. Unafikiri hadithi hii inahusu nini? Picha inakuambia nini ambacho kitakusaidia kutabiri hadithi hii inahusu nini? (Mwalimu aruhusu majibu mengi kutoka kwa wanafunzi na awatie moyo juu ya majibu yao – Ni muhimu kwa mwalimu kutowaambia wanafunzi kuwa wamekosea kwani hiyo itawavunja moyo, na inaweza kupunguza kujiamini kwao – Ni muhimu pia mwalimu asitoe majibu kwa wanafunzi, mwalimu asubiri kidogo na atumie muda huo kuhamasisha wanafunzi kujibu kwa kadiri wanavyofahamu.)*
>
> *Kwa kawaida katika hadithi zetu tunaweza kuona tatizo au fundisho la kujifunza kutoka kwa wahusika katika hadithi husika. Unafikiri ni nini linaweza kuwa ni tatizo baina ya Sungura na Kobe katika hadithi yetu tunayoisoma leo? Je ni mafunzo gani tunayoweza kupata kutoka katika hadithi hii? (Hapa pia mwalimu anaweza kukubaliana na utabiri wa wanafunzi kuhusu hadithi hiyo. Mwalimu asubiri kidogo na muda huo kuhamasisha utabiri zaidi kutoka kwa wanafunzi.)*
>
> *Ni hadithi gani nyingine tulizosoma kuhusu wanyama zinazo fanana na hadith yetu ya leo? Unakumbuka nini kuhusu hadithi hizo? (Kwa mara nyingine tena mwalimu asaidie majadiliano kuendelea na atoe muda ili kuhamasisha wanafunzi kuongea)*
>
> *Inaonekana tuna mawazo mengi kuhusu tutakachokuwa tukisoma leo. Sasa tafuta mwenzako wa Kusoma nae na msome hadithi kwa pamoja. Kumbuka mnasoma kimya. Hii itawasaidia kuikumbuka hadithi vizuri zaidi. Kama kuna tatizo lolote la Kusoma maneno au kueleawa, nyoosha mkono ili nikusaidie. Pia kumbuka kuwa tutazungumza juu ya hadithi hii baada ya Kusoma, hivyo ni muhimu kukumbuka kila kitu unachoweza katika hadithi hii. Sasa tusome, na kuona kama utabiri wetu na mawazo yetu ni sahihi.*

Kuandaa wanafunzi kabla ya kusoma, wanaweza kutabiri hadithi inayofuata, akili zao huwa ni changamfu na huwa tayari kusoma, na wataelewa matini kwa usahihi zaidi. Walimu wasipowaandaa wanafunzi kabla ya kuanza kusoma, wanafunzi hawatakuwa na

hakika kuhusu watakachosoma, na jambo la muhimu ni kuwa hawana hakika kuhusu hasa ni kwa nini wanasoma.

## Mambo ya Kufanya na Kutofanya Wakati wa Kusoma

*Mambo ya kufanya*

1. Tambulisha matini kwa wanafunzi
2. Onyesha picha yoyote au taswira yoyote itakayowasaidia wanafunzi kutabiri kuhusu matini
3. Uliza maswali ili kuwasaidia wanafunzi kufanya utabiri kuhusu matini
4. Tumia majadiliano kuongeza motisha ya wanafunzi kusoma

*Mambo ya Kutofanya*

1. Usiwape watoto mtihani rasmi wa kuwapima kuhusiana na matini
2. Usiwasomee wanafunzi matini
3. Usiwape zoezi lolote linalohusiana na matini , isipokuwa kuisoma matini
4. Usiwaandae wanafunzi kusoma kwa sauti
5. Usitoe mrejesho hasi wakati wa majadiliano au utabiri wa wanafunzi

## Wakati wa kusoma

Wakati wa kusoma, wanafunzi wanatakiwa kusoma kimya (wakati wote wa kusoma matini). Kusoma kimya kunawawezesha wanafunzi kulenga kupata kufahamu wa kile wanachosoma. Wanafunzi wanaposoma kwa sauti mtazamo wao hauwi kwenye kuelewa wanachosoma. Mtazamo wao unakuwa kwenye kusoma maneno kwa usahihi. Hii ni kwa sababu, Kusoma kwa sauti hakusaidii kujenga ufahamu, na pia hufifisha uwezo wa wanafunzi kufahamu matini wanayosoma. Wakati wanafunzi wanasoma, mwalimu anatakiwa awe kimya lakini awe anawaangalia ili kuona tabia zifuatao:

1. Kusoma kutoka mbele kwenda nyuma ya matini.
2. Kusoma kimya (wanafunzi wanaweza kuwa wanachezesha midomo yao, hii waruhusiwe)
3. Kuwatazama wanafunzi ambao watanyoosha mkono kwa kuwa na ugumu au maswali kuhusu matini.

Wanafunzi wanapohitaji msaada wa mwalimu wakati wa kusoma, wasaidiwe bila kusumbua wengine darasani, hivyo jambo hili lifanyike kwa utulivu wa hali ya juu. Msaada unatakiwa uwe wa haraka na kwa wakati, na ujumuishe vitu kama:

1. Kutoa ufafanuzi kuhusu maneno mapya na yenye utata ambayo yanawafanya wanafunzi wasiwe katika mwendelezo wa kusoma
2. Kujibu swali lolote (linalohusiana na usomaji) ambalo wanafunzi wanaweza kuuliza.

## Mambo ya Kufanya na Kutofanya Wakati wa Usomaji

*Mambo ya Kufanya*

1. Tarajia na hakikisha usomaji wa kimya unafanyika
2. Fuatilia kuhakikisha wanafunzi wanasoma kuanzia mbele kwenda nyuma na kutoka kushoto kwenda kulia.
3. Angalia wanafunzi ambao wanaopata shida kusoma na uwape msaada
4. Hakikisha msaada ni wa haraka na kwa wakati

*Mambo ya Kutofanya*

1. Usiwaingilie wanafunzi wanaposoma kimya kwa masahihisho au maoni katika kikundi chochote
2. Usitumie muda mwingi kwa wanafunzi wanaohitaji msaada , fanya haraka na kwa wakati
3. Usimtoe mwanafunzi yeyote kwenye kipindi cha kusoma ili akafanye shughuli nyingine

### Baada ya Kusoma

Baada ya kusoma ni sehemu muhimu sana katika somo la kusoma kwa ufahamu. Huu ni wakati ambao wanafunzi hutafakari uelewa wao wa matini, kupata ufafanuzi kutokana na majadiliano, na kujenga kujiamini katika kusoma huru. Kwa kuongeza, huu ni Wakati ambao walimu wanaweza kupata taarifa zaidi kuhusu ubora wa mwanafunzi katika uwezo wake wa kusoma – ambapo wanaweza kujiuliza swali "Je wanafunzi wanaelewa wanachosoma?"

Mchakato wa baada ya kusoma unatakiwa kujumuisha mambo makuu mawili: 1) Kuuliza na kujibu maswali na 2) Kujibu matini kiubunifu.

*Kuuliza na Kujibu Maswali:* Kwa wanafunzi wachanga, walimu wanatakiwa kuuliza maswali rahisi. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuuliza kuhusu majina ya wahusika, kichwa cha habari, mahali tukio lilipotokea. Walimu hawatakiwi kuuliza maswali ya ngazi ya juu. Wanafunzi wenye umri mchanga wanatakiwa kusoma matini rahisi, lakini kwa kawaida wana uwezo wa kujibu ngazi ya juu ya maswali na inapaswa wahamasishwe kufanya hivyo.

Sampuli ya jedwali la kiwango cha chini – kati na juu cha maswali ni kama ifuatavyo:

| Kiwango cha Chini cha Maswali | Kiwango cha Kati cha Maswali | Kiwango cha Juu cha Maswali |
|---|---|---|
| Kichwa cha habari cha hadithi ni nini?<br><br>Jina la mhusika mkuu ni nani?<br><br>Wahusika wa hadithi hii | Kimetokea nini mwanzo wa hadithi?<br><br>Ni tatizo gani limejitokeza kati ya wahusika?<br><br>Kulijitokeza nini mwisho | Ni kwa kiasi gani wahusika wameweza kutatua tatizo?<br><br>Umepata funzo gani?<br><br>Umejifunza nini kutokana na |

| | | |
|---|---|---|
| wako wangapi? | wa hadithi? | hadithi hii? |

Ili kuweza kutoa kiwango cha juu cha ubora katika somo la kusoma kwa ufahamu, walimu ni lazima waandae maswali ya kuuliza kabla ya kuanza kwa somo. Kama hii haitafanyika utakosa nafasi ya kuuliza kiwango cha juu cha maswali ambayo yana changamoto kwa wasomaji wenye umri mchanga

*Kujibu Matini kwa Kiubunifu:* Kujibu matini kwa kiubunifu ni tofauti na kujibu maswali katika mjadala. Kujibu kwa kiubunifu kunajumuisha shughuli shirikishi ambazo zinawasaidia wanafunzi kufurahia matini na kukuza uelewa wao katika matini husika, hivi ni vitu muhimu katika makuzi ya wasomaji wachanga. Hapa chini ni baadhi ya mifano michache:

1. Kuchora picha za wahusika wawapendao au sehemu ya hadithi wanayoipenda
2. Kuandika hitimisho la mwisho wa hadithi kwa namna nyingine kwa kushirikiana na mwalimu
3. Kuweka michoro iliyochorwa na wanafunzi katika vikundi inayo onyesha lengo kuu au maudhui makuu ya hadithi
4. Kutengeneza kadi za misamiati (kwa ajili ya kuweka katika kuta za darasa) mipya na muhimu inayotokana na hadithi husika
5. Kutengeneza vikaragosi ya wahusika wakuu kutokana na hadithi waliyosoma na pia kufanya maigizo mafupi kutokana na hadithi husika
6. Kurudia kuisoma hadithi kwa sauti (kufanya zoezi la ufasaha)

Walimu wanaweza kuogopa kwamba maswali na majibu yanaweza kupoteza muda wa kufundisha. Lakini ni vizuri kutambua kuwa maswali na majibu husaidia kuhakikisha kuwa wanafunzi wanaelewa vizuri maudhui ya matini, inaongeza hamasa kwa watoto, na pia husaidia wanafunzi kupenda Kusoma katika maisha yao.

## Baada ya Kusoma: Vitu vya Kufanya na Vitu vya Kutofanya

*Vitu vya Kufanya*

1. Baada ya Kusoma matini washirikishe vizuri wanafunzi
2. Husisha maswali ya ngazi ya chini, ya kati na ya juu katika mijadala yote ya usomaji
3. Wahamasishe wanafunzi kutengeneza vitu mbali mbali kama mrejesho wa kile walichosoma.

*Vitu vya kutofanya*

1. Usitegemee wanafunzi wachanga kujibu maswali yaliondikwa au wajibu maswali kwa kuandika
2. Usitahini wanafunzi uelewa wa kile walichosoma, tabia ya kutahini punde tu baada ya Kusoma hupunguza hamasa ya wanafunzi kusoma

## Kupanga kwa ajili ya Ufundishaji wenye Ufanisi wa Kusoma kwa Ufahamu

Walimu siku zote wapange/waandae mapema somo lolote la Kusoma kwa Ufahamu. Andalio la somo linaweza kuwa rahisi lakini lazima liwe na taarifa zifuatazo:

1. Stadi za msingi zitakazofundishwa katika somo husika (angalia orodha ya ujuzi hapo juu)
2. Matini itakayotumika, ngazi ya matini hiyo (kufaa kwake kwa wanafunzi) na ufupisho wa matini hiyo (mwalimu lazima asome matini hiyo kabla ya kuitumia darasani.)
3. Mikakati kadhaa ya kuandaa wanafunzi kabla ya kusoma.
4. Maswali ya kuuliza wanafunzi baada ya kusoma.
5. Mkakati mmoja wa wanafunzi kuijibu matini baada ya kusoma.

### Mfano wa Andalio la Somo la Kusoma

| | |
|---|---|
| **Tarehe ya Somo** | |
| **Stadi za Kusoma tunazoshughulikia leo** | ☐ Kubashiri<br>☐ Kutambua wahusika<br>☐ Tatizo na ufumbuzi<br>☐ Sababu na athari<br>☐ Mtiririko wa matukio<br>☐ Kusimbua maneno ambayo hayajazoeleka<br>☐ Kutumia picha, michoro na chati<br>☐ Kuelewa matini yenye taarifa<br>☐ Ukweli na maoni<br>☐ Wazo kuu<br>☐ Kusoma maneno yaliyozoeleka |
| **Kichwa cha habari cha matini** | |
| **Ngazi ya matini** | |
| **Ufupisho wa matini** | |
| **Mbinu za kabla ya kusoma** | |
| **Mikakati ya kufanya onesho la usomaji** | Itumike tu pale onesho linapofanyika |
| **Maswali baada ya kusoma** | Ngazi ya chini<br>Ngazi ya kati<br>Ngazi ya juu |
| **Mikakati ya kujibu matini** | |

## Kutoa msaada kwa wanafunzi wenye shida ya kusoma.

Hata kama walimu wanafundisha kwa ubora wa juu usomaji, kwa kushirikisha vipengele vyote muhimu, na kuweka uwiano wa muda katika kufundisha, bado kuna wanafunzi watakaohangaika ili kuwa wasomaji wazuri. Hii inatokea kwa sababu mbalimbali: wakati mwingine wanafunzi walianza vibaya maisha yao ya shuleni, na kupata maandalizi hafifu ya kujifunza. Wakati mwingine ni kwa sababu mwanafunzi binafsi hajakomaa kiutambuzi na kihisia kuliko anavyotakiwa kuwa, na hivyo kujifunza taratibu zaidi. Wakati mwingine wanafunzi wanakuwa na ulemavu wa kujifunza ambao huchukua muda kuuona, na ili kushughulikiwa kwa kutumia njia maalum za kufundishia.

Walimu wanaofuata mbinu za kusoma kwa ufahamu zilizooneshwa hapo juu wataweza kukusanya ushahidi utakao wasaidia kufahamu ni wakati gani mwanafunzi anapata ugumu katika kusoma. Na walimu watawajibika kutoa maelekezo ya kumsaidia mwanafunzi. Hii inaweza kukamilishwa kwa njia tofauti:

1. ***Kurekebisha matini –*** yawezekana kiwango cha matini kinachotumika ni kigumu kwa mwanafunzi. Jaribu kutumia kitabu ambacho ni rahisi, na tazama kama ufahamu wa mwanafunzi unaboreka.

2. ***Kutoa msaada darasani*** – wakati wanafunzi wengine wanafanya kazi wenyewe katika viti vyao, kaa karibu na mwanafunzi anayepata shida kusoma, mwambie asome kwa sauti ili kusikiliza usimbuzi wake wa maneno na sauti, na msamiati, waambie kusoma pamoja na wewe-sikiliza kama wanaweza kumudu kasi, kupanda na kushuka kwa sauti kama unavyosoma wewe, na wasahihishe kadri wanavyosoma. Ongea nao kuhusu jambo unalosoma nao. Hii itasaidia kutambua mambo na kujenga kujiamini kwa mwanafunzi kadri anavyoendelea kupata msaada.

3. ***Jozi ya wenza wanaosoma kwa ufasaha*** –mweke mwanafunzi anayehaingaka kusoma pamoja na yule anayesoma kwa ufasaha. Wanafunzi wanaosoma vema huwa ni mfano kwa wale wanasoma kwa shida. Kwa kuweka pamoja mwanafunzi anayesoma kwa ufasaha na yule anayesoma kwa shida, mwanafunzi anayesoma kwa shida atajifunza jinsi ya kumudu kusoma na kuelewa matini.

4. ***Subiri–*** wakati mwingine huchukua muda kwa mwanafunzi anayeanza taratibu kufanya vizuri. Tumia mbinu bora za kufundisha na subiri mwanafunzi ajifunze ujuzi husika. Wanafunzi wengi hawana ulemavu wa kujifunza, na hatimaye wataendelea vizuri kuliko wanafunzi wengine wote.

Ikiwa matumizi ya mbinu za kufundisha mwanafunzi anayepata shida kusoma zitashindwa, mwanafunzi atahitaji kupelekwa katika rufaa, kupimwa ili kutumia mbinu maalumu zaidi za kufundishia.

# VIAMBATISHO: Mifano ya Masomo ya Kusoma kwa Ufahamu

## Mfano wa Andalio la Somo # 1: Onesho la Mfano kwa Wasomaji Wanaoanza

| | |
|---|---|
| **Tarehe ya Somo** | Januari 21, 2015 |
| **Stadi za kusoma tunazoshughulikia leo** | ✓ Kubashiri<br>☐ Kutambua wahusika<br>✓ Tatizo na ufumbuzi<br>☐ Sababu na athari<br>☐ Mtiririko wa matukio<br>☐ Kusimbua maneno ambayo hayajazoeleka<br>✓ Kutumia picha, michoro na chati<br>☐ Kuelewa matini yenye taarifa<br>☐ Ukweli na maoni<br>☐ Wazo kuu<br>☐ Kusoma maneno yaliyozoeleka |
| **Kichwa cha habari cha matini** | Safari ya kwenda nyumbani kwa Bibi |
| **Ngazi ya matini** | Wasomaji wanaoanza. Kitabu cha picha bila maneno |
| **Ufupisho wa matini** | Kitabu hiki kinahusu kisa cha msichana mdogo ambaye alimtembelea bibi yake. Alipokuwa akienda kwa Bibi yake njiani akapotea na kuhitaji msaada. Mwisho anakutana na mzee moja anayemjua Bibi yake na akamsaidia kufika nyumbani kwa Bibi yake. |
| **Mbinu za kabla ya kusoma** | Tambulisha kitabu kwa kusoma kichwa cha kitabu kwa sauti. Chunguza picha kwenye jalada la kitabu.<br><br>*Maswali:* Unafikiri kitabu hiki kinahusu nini?. Fanya ubashiri na uwatake wanafunzi pia kufanya ubashiri. |
| **Mikakati ya kufanya onesho la mfano wa usomaji** | *Kila Ukurasa:* Sema kwa sauti kuhusu picha, zinatuambia nini?<br>Katikati ya kitabu, uliza swali- ni watu wangapi alikutana nao njiani? Bashiri kisha rudi katika ukurasa na kuhesabu pamoja na wanafunzi. Bainisha tatizo lilikuwa ni nini? Chunguza kubashiri kwa wanafunzi walikofanya mwanzo kabla ya kusoma<br>*Uliza swali* – Sijui atafikaje kwa Bibi yake? Waulize wanafunzi wabashiri. |
| **Maswali baada ya kusoma** | **Ngazi ya chini**<br>Kitabu/Hadithi ilihusu nini?<br>**Ngazi ya kati**<br>Ni nani waliandikwa katika kitabu/hadithi? Unajua nini kuhusu wahusika?<br>**Ngazi ya juu**<br>Ni tatizo gani lililompata msichana? Alilitatuaje? Kitu kama hiki kiliwahi kukutokea wewe pia? Je ulikitatuaje? |
| **Mikakati ya kujibu matini** | Wanafunzi wamchore mhusika mojawapo anayewafanya wakumbuke kitu Fulani kuhusu huyo mhusika. Sema kuhusu picha zao na mzibandike ukutani. |

## Mfano wa Andalio la Somo # 2: Kufundisha Kikundi Kizima cha Wasomaji Wanaoanza

| | |
|---|---|
| **Tarehe ya Somo** | Januari 23, 2015 |
| **Stadi za kusoma tunazoshughulikia leo** | ☐ Kubashiri<br>☐ Kutambua wahusika<br>✓ Tatizo na ufumbuzi<br>☐ Sababu na athari<br>✓ Mtiririko wa matukio<br>☐ Kusimbua maneno ambayo hayajazoeleka<br>✓ Kutumia picha, michoro na chati<br>☐ Kuelewa matini yenye taarifa<br>☐ Ukweli na maoni<br>☐ Wazo kuu<br>✓ Kusoma maneno yaliyozoeleka |
| **Kichwa cha habari cha matini** | Safari ya kwenda nyumbani kwa Bibi |
| **Ngazi ya matini** | Wasomaji wanaoanza. Kitabu cha picha bila maneno |
| **Ufupisho wa matini** | Kitabu hiki kinahusu kisa cha msichana mdogo ambaye alimtembelea bibi yake. Alipokuwa akienda kwa Bibi yake njiani akapotea na kuhitaji msaada. Mwisho anakutana na mzee moja anayemjua bibi yake na akamsaidia kufika nyumbani kwa bibi yake. |
| **Mbinu za kabla ya kusoma** | **Maswali:** Nani anakumbuka kitabu hiki? Kichwa cha kisa hiki ni kipi? Unakumbuka nini kuhusu kisa hiki?<br><br>Leo tutasoma kisa katika kitabu hiki pamoja. Kumbuka kuwa kitabu siyo lazima kuwa na maneno ili tukielewe. Tunaweza kutumia picha kuelewa kisa au hadithi na hata kuielezea sisi wenyewe.<br><br>Nitawaonyesha kitabu kwenye projekta ukurasa kwa ukurasa. Kaa karibu na mwenzako na kila ukiona picha mweleze mwenzako kisa kuhusu picha hiyo kwa maneno yako mwenyewe. |
| **Mikakati ya kufanya onesho la usomaji** | hakuna |
| **Maswali baada ya kusoma** | **Ngazi ya chini**<br>Je ulisimulia hadithi/kisa vile vile na ulivyoisimulia katika somo lililopita?<br>**Ngazi ya kati**<br>Usimuliaji wako wa Hadithi ulikuwa ni ule ule kwa kiwango gan? Ulikuwa tofauti kwa Kiwango gani?<br>**Ngazi ya juu**<br>Ni maneno yapi uliyoyatumia mara kwa mara katika hadithi/Kisa ulichosimulia? Ni Bibi au Mtoto? Hebu tubandike hayo maneno ukutani, ili tuyaone tena wakati tutakaposoma hadithi/kisa |

| | |
|---|---|
| **Mikakati ya kujibu matini** | Andika kisa/hadithi kwa kutumia picha. Tumia karatasi ya chati na kalamu za makapeni kutengeneza hadithi (fupi) kwa kutumia picha tu.<br>Unataka hadithi kuhusu nini?<br>Kipi kinaanza kwanza? Kipi kinachofuata…?<br>Tusome picha tena. Je hadithi inaleta maana?<br>Tuhitimishe hadithi kwa kuipa kichwa. Je unafikiria kichwa cha hadithi kiwe kipi?<br>Bandika hadithi ya picha ukutani. |

## Mfano wa Andalio la Somo # 3: Onesho la Mfano kwa Wasomaji Wanaoibukuia

| | |
|---|---|
| **Tarehe ya Somo** | Februari 15, 2015 |
| **Stadi za kusoma tunazoshughulikia leo** | ✓ Kubashiri<br>☐ Kutambua wahusika<br>☐ Tatizo na ufumbuzi<br>☐ Sababu na athari<br>✓ Mtiririko wa matukio<br>✓ Kusimbua maneno ambayo hayajazoeleka<br>✓ Kutumia picha, michoro na chati<br>✓ Kuelewa matini yenye taarifa<br>☐ Ukweli na maoni<br>✓ Wazo kuu<br>✓ Kusoma maneno yaliyozoeleka |
| **Kichwa cha Habari cha matini** | Shambani |
| **Ngazi ya matini** | Darasa la kwanza - muhula pili – Matini ya taarifa, maneno yaliyozoeleka, na ya kusimbua (decoding) |
| **Ufupisho wa matini** | Hii ni hadithi ya kusimbua maneno ya awali inayohusisha picha na neno moja kwa kila ukurasa. Kila ukurasa unaonyesha shughuli inayofanyika shambani. Inaonyesha shughuli za mkulima kwa siku na kwa mpangilio sahihi. Hadithi inaweza kutumika kufundisha mtiririko wa matukio na kujifunza maneno mapya. |
| **Mbinu za kabla ya kusoma** | *Kutambulisha Hadithi:* Kichwa cha hadithi ni kipi? Je kichwa cha hadithi kina neno/maneno mapya kwa wasomaji? Nani anaweza kusoma kichwa cha hadithi? Unafikiri hadithi inahusu nini? Kwa nini? Nitawasomea hadithi nikiwaonyesha jinsi msomaji anavyofikiria. Kumbuka mtiririko wa matukio yanavyotokea. |
| **Mikakati ya kufanya onesho la usomaji** | Soma kila ukurasa, sema kwa sauti kuhusu picha. Kila ukurasa soma maneno na zungumzia maneno tunayoyafahamu kwa sauti na tamka maneno tusiyoyajua (onyesha tabia ya kusimbua). |

| | |
|---|---|
| | Simama katikati ya hadithi, na sema kwa sauti kuhusu mtiririko wa matukio katika hadithi. Rudi nyuma ya hadithi na onyesha namna msomaji anavyokumbuka mpangilio wa matukio, |
| **Maswali baada ya kusoma** | **Ngazi ya chini**: Je tulikuwa sahihi kubashiri hadithi inahusu nini?<br><br>**Ngazi ya kati** Je unaweza kukumbuka mtiririko (mpangilio) wa kazi ya mkulima katika hadithi hii? Eleza kilicho fanyika kwanza, ni kitu gani kilichofuata….<br><br>**Ngazi ya juu:** Kwa nini ni muhimu kukumbuka mtiririko wa matukio wakati tunaposoma hadithi? |
| **Mikakati ya kujibu matini** | Tutafanya kazi pamoja kusimulia tena hadithi hii katika mpangilio wake sahihi. Tutatumia maneno kuandika hadithi kwenye karatasi ya chati.<br><br>Hebu tujaribu kutumia maneno tunayoyajua na maneno mengine mapya tuliyoyasoma kwenye hadithi. Tunaweza pia kuandika maneno hayo mapya kwenye kadi na kubandika ukutani ili tuyakumbuke tutakaposoma tena. |

## Mfano wa Andalio la Somo #4: Usomaji katika Kikundi kidogo. Msomaji anayeibukia

| **Tarehe** | Februari 16, 2015 |
|---|---|
| **Stadi za kusoma tunazoshughulikia leo** | ☐ Kubashiri<br>☐ Kutambua wahusika<br>☐ Matatizo na suluhisho<br>☐ Sababu na athari<br>✓ Mtiririko wa matukio<br>✓ Kusimbua maneno yasiyozoeleka<br>✓ Matumizi ya picha, chati na grafu<br>✓ Kuelewa matini yanayotoa taarifa<br>☐ Ukweli na maoni<br>☐ Wazo kuu<br>✓ Kusoma maneno yasio zoeleka |
| **Kichwa cha habari cha matini** | Shambani |
| **Ngazi ya matini** | Darasa la kwanza, muhula wa pili– matini ya taarifa, maneno yaliyozoeleka na maneno ya kusimbuliwa. |
| **Ufupisho wa matini** | Hadithi ni ya usimbuzi wa maneno ya awali, ni pamoja na picha maneno mafupi kwenye kurasa. Kila ukurasa unaonesha kazi iliyofanyika shambani. Inaonesha kazi za kila siku za shambani kwa mpangilio sahihi. |
| **Mikakati ya kabla ya kusoma** | Je, nani anajua hadithi tuliyosoma jana? Unakumbuka nini kuhusu hadithi hiyo? Jadili. Leo mtasoma pamoja katika makundi madogo. Kila mtu katika kikundi atasoma ukurasa mmoja, kwa kutumia picha na maneno kwa pamoja atuambie |

| | |
|---|---|
| | kilichotokea katika ukurasa huo aliosoma. Baada ya kusoma, nitakuuliza maswali ambayo utajibu katika kundi. Kisha tutashirishana kuona majibu ili kuona ni nani anakumbuka hadithi hiyo. |
| **Mikakati ya kufanya onesho la kusoma** | Hakuna |
| **Maswali baada ya kusoma** | Haya maswali yanaulizwa katika vikundi vidogo, kisha vikundi hujadili majibu yake na kisha kushirikisha darasa zima.<br><br>**Ngazi ya chini:** Je unafikiri wazo kuu katika hadithi hii nini, kwa kiasi kikubwa inahusu nini?<br><br>**Ngazi ya kati:** Je ni maneno gani yaliyozoeleka uliyoyaona katika kitabu? Je ni maneno gani yaliyozoeleka uliyoyaona na kuyasoma ambayo hayakuwa katika kitabu?<br><br>**Ngazi ya juu**: Ni maneno gani mapya umesoma leo? Ni kwa jinsi gani ulitumia herufi na sauti kutamka maneno na kujua maana zake? |
| **Mkakati wa kujibu matini** | Katika kikundi kidogo,unavyo bango, karatasi na makapeni.Tazama hadithi, chukua neno moja unalolifahamu na unataka kulibandika ukutani-neno muhimu ambalo utalisoma mara kwa mara. Kisha chukua neno moja ambalo hukulifahamu kabla na ambalo ni muhimu kujifunza. Shirikisha darasa zima na kisha libandike ukutani |

## Mfano wa Andalio la Somo #5: Kuonesha Mfano kwa Wasomaji Mahiri

| | |
|---|---|
| **Tarehe ya Somo** | 2 Mei 2015 |
| **Stadi za kusoma tunazoshughulikia leo** | ☐ Kubashiri<br>☐ Kutambua wahusika<br>☐ Tatizo na ufumbuzi<br>✓ Sababu na athari<br>☐ Mtiririko wa matukio<br>✓ Kusimbua maneno ambayo hayajazoeleka<br>✓ Kutumia picha, michoro na chati<br>✓ Kuelewa matini yenye taarifa<br>☐ Ukweli na maoni<br>✓ Wazo kuu<br>✓ Kusoma maneno yaliyozoeleka |
| **Kichwa cha habari cha matini** | Mashine Rahisi |
| **Ngazi ya matini** | Darasa la pili, muhula wa pili – Kitabu cha kiada cha sayansi |
| **Ufupisho kuhusu matini** | Ni usomaji mfupi kutoka katika kitabu cha kiada cha Sayansi kuhusiana na aina za mashine rahisi na madhumuni yake. Kitabu hiki ni kizuri katika kuzungumzia chanzo na matokeo, kutumia picha kupata Ufahamu, na kuelewa tofauti kati ya riwaya na taarifa. |
| **Mbinu kabla ya** | Tambulisha matini: Kichwa cha habari cha matini hii ni nini? Unadhani matini hii |

| | |
|---|---|
| **kusoma** | ni ya hadithi au inahusu taarifa? Umejuaje? Leo, nitasoma matini hii kwa sauti, na kuwaonesha ni kwa namna gani wasomaji hutumia michoro au picha kuelewa zaidi kuhusu taarifa wanazosoma. Sikilizeni na mtazame nitakavyokuwa nasoma kwa sauti. |
| **Mbinu za kuonesha mfano** | Soma kila ukurasa. Simama kusoma katika kila mchoro wa mashine rahisi, soma kila maandishi (lebo) yaliyo kwenye mchoro, fikiri kwa sauti kuhusu kila picha na jinsi inavyoonyesha sehemu zake na jinsi zinavyofanya kazi. |
| **Maswali baada ya kusoma** | **Ngazi ya chini:** Leo tumesoma kuhusu mashine gani rahisi?<br><br>**Ngazi ya kati:** Baadhi ya sehemu tulizoona kwenye mchoro ambazo hufanya mashine rahisi ifanye kazi ni zipi?<br><br>**Ngazi ya juu:** Ni kwa namna gani michoro hiyo imeweza kutupatia taarifa zaidi kuliko matini tuliyosoma? Unasomaje michoro? |
| **Mikakati ya kujibu matini** | Vipe vikundi kazi ya kuchora mashine rahisi. Waulize watumie matini kama mfano, na waweke lebo katika mashine rahisi zao. Onyesha mchoro kwa darasa zima na mjadili. |

## Mfano wa Andalio la Somo #6: Kufundisha Kundi Zima la Wsaomaji Mahiri

| | |
|---|---|
| **Tarehe ya Somo** | 3 Mei 2015 |
| **Stadi za kusoma tunazoshughulikia leo** | ☐ Kubashiri<br>☐ Kutambua wahusika<br>☐ Tatizo na ufumbuzi<br>✓ Sababu na athari<br>☐ Mtiririko wa matukio<br>✓ Kusimbua maneno ambayo hayajazoeleka<br>✓ Kutumia picha, michoro na chati<br>✓ Kuelewa matini yenye taarifa<br>☐ Ukweli na maoni<br>✓ Wazo kuu<br>✓ Kusoma maneno yaliyozoeleka |
| **Kichwa cha habari cha matini** | Mashine rahisi |
| **Ngazi ya matini** | Darasa la pili, muhula wa pili – Kitabu cha kiada cha Sayansi |
| **Ufupisho kuhusu matini** | Ni usomaji mfupi kutoka katika kitabu cha kiada cha Sayansi kuhusiana na aina za mashine rahisi na madhumuni yake. Kitabu hiki ni kizuri katika kuzungumzia chanzo na matokeo, kutumia picha kupata Ufahamu, na kuelewa tofauti kati ya riwaya na taarifa. |
| **Mbinu za kabla ya kusoma** | Rudi kwenye kundi lako na michoro uliyochora jana. Nani anaweza kutaja aina zote za mashine rahisi tulizojifunza jana? Ni kitu gani muhimu ambacho tunapaswa kujua kuhusu mashine hizo? Leo mtasoma kifungu cha habari kutafuta taarifa muhimu za Kuelezea kubuni na kutumia mashine rahisi yako. Soma kifungu chote cha habari. |
| **Mswali baada ya** | **Kiwango cha chini:** Umejifunza nini kuhusu mashine rahisi yako? |

| | |
|---|---|
| **kusoma** | **Kiwango cha kati:** Ni taarifa gani muhimu kuhusu hiyo mashine? Ni taarifa gani ambayo si muhimu sana?<br><br>**Kiwango cha juu:** Mashine yako inafanyaje kazi? Ni kitu gani kinasababisha ifanye kazi vizuri? |
| **Mikakati ya kujibu matini** | Fanyeni kazi katika makundi yenu kuandika taarifa muhimu kuhusu mashine yako. Baada ya kuandika taarifa nzuri, ihamishie kwenye mchoro uliochora jana. Tutashirikishana darasani na kuweka picha zako katika kitabu chetu cha maktaba ya darasa. |